

**N**chi za Afrika zinakimbilia kuwapa wazalishaji wa mimea haki zenye nguvu za umiliki (haki za wazalishaji wa mimea) juu ya mbegu na vipandikizi. Huu ndio utakuwa mwisho wa mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima wenyewe. Serikali za Afrika zinafanya hivi kwa kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaoitwa Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina za Mimea (UPOV 1991). Muungano wa UPOV ulitayarishwa na wazalishaji wa mimea kutoka Ulaya kwa ajili ya mifumo ya kilimo iliyo na matumizi makubwa ya viwanda.

Mkataba wa UPOV 1991 haufai kwa kilimo cha Afrika, ambacho mbegu nyingi zinazotumika ni zile zilizohifadhiwa kutoka shamba. Mbegu za biashara zinafaa kwa kilimo kikubwa cha zao moja na hutegemea matumizi ya umwagiliaji, pia viuadudu na mbolea za kemikali ambazo ni ghali na zenye madhara.



# HAKI ZA WAZALISHAJI WA MIMEA, HAKI ZA WAKULIMA NA UPOV 1991

Wakulima wadogo wanapopanda mbegu zinazolindwa na Mkataba wa Haki za Wazalishaji, watalazimika kununua mbegu kila msimu. Hawataweza kuhifadhi mbegu kutokana na mavuno yao ili washirikiane, wauziane au kubadilishana na familia zao, marafiki na jamii yao. Kununua mbegu kila mwaka kutasababisha deni na utegemezi mkubwa kwenye mbegu za kibiashara. Hii pia itapelekea kupoteza uanuwai wa mbegu na uhuru wa wakulima. Serikali nyingi za Afrika wamelifanya kuwa kosa la jinai kwa wakulima kurudia kupanda au kubadilishana mbegu ambazo aina zake zinalindwa.

Aina ya kilimo kinachowafaa zaidi wakulima wadogo ni kile kinachowapa wakulima udhibiti. Ni kile ambacho kinatumia mbegu anuwai zilizoendelezwa na wenyeji zinazozalisha aina nyingi tofauti za mazao kwa ajili ya lische na chakula cha mifugo.

